

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"
Telephone: + 028 2750271
Fax: + 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

Kumb.Na.MDC/ADM/5/13/Vol.II/99

17.10.2017

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI KWA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Maswa anawatangazia wananchi wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya wilaya ya Maswa nafasi za kazi ya mkataba kama ifuatavyo:

1.Afisa Masoko Msaidizi – Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

- (a) Awe na elimu ya Kidato cha IV au VI
- (b) Awe na Astashahada ya Kwanza katika fani ya Masoko
- (c) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (d) Awe na cheti cha kuzaliwa

Kazi za kufanya

- Kutafuta masoko ya chaki
- Kuratibu na kusimamia mauzo ya Chaki kwenye masoko
- Kuandaa nyaraka zote zinazohusu mauzo
- Kutoa taarifa ya hali ya soko na mauzo kwa Kamati tendaji kila mwezi
- Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uboreshaji wa soko na uongezaji wa mauzo.
- Kuwajibika kwa Kamati Tendaji

- Kukusanya na kuandaa taarifa za Masoko (market information system) na kuziwasilisha kwenye Kamati tendaji.
- Kusimamia, kusambaza na kuuza chaki katika maeneo yote ya masoko
- Kutangaza ubora wa bidhaa zetu kwa wateja
- Kutafuta masoko mapya na kuongeza mauzo kwenye kiwanda kila mwezi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

Mshahara

Mshahara kwa kazi hii utakuwa sh.**390,000** kwa mwezi .

Kituo cha kazi

Atafanya kazi katika kiwanda cha Chaki kilichopo Halmashauri ya wilaya ya Maswa.

2. Mfamasia Msaidizi – Nafasi 1

Sifa za Mwombaji

- (a) Awe na elimu ya Kidato cha IV au VI
- (b) Awe na Stashahada katika fani ya Ufamasia
- (c) Awe na umri usiozidi miaka 45
- (d) Awe na cheti cha kuzaliwa

Kazi za kufanya

- Kuainisha mahitaji ya mwaka ya dawa na vifaa na kuandaa bajeti yake.
- Kuagiza, kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa na vifaa tiba.
- Kutunza kumbukumbu za dawa
- Kuandaa orodha ya dawa za hospitali

- Kutoa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa
- Kusimamia matumizi sahihi ya dawa
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

Mshahara

Mshahara kwa kazi hii utakuwa sh. **680,000** kwa mwezi .

Kituo cha kazi

Atafanya kazi katika duka la dawa lililopo katika Hospitali ya wilaya ya Maswa.

MUDA WA MKATABA

Mkataba wa kazi hizi utakuwa ni mwaka mmoja mmoja na unaweza kurudiwa (renewed) kwa kuzingatia utendaji kazi wa mtumishi husika.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua za Maombi zitumwe kwa:
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P 170,
Maswa –Simiyu.

Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma na Cheti cha kuzaliwa. Wataoitwa kwenye usaili wafike na vyeti halisi (Original certificates).

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/10/2017 saa 9.30 alasiri.

Dr.Sagamiko F.D
**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA.**